**SHULE YA SEKONDARI MGUGU,**
**S.L.P 1568,**
**MOROGORO.**
**TAREHE……………………**

**KUMB;Na MGSS/JI/FI/20…….**
**MKUU WA SHULE: 0789 120 720**
**MAKAMU MKUU WA SHULE 0624 611 447**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………….............................................**
**S.L.P……………………………**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA, 2026 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MGUGU ILIYOPO WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninayofuraha kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka wa masomo **2026** katika shule hii. Shule ya Sekondari ya Mgugu ipo umbali wa km 100 kutoka Morogoro Mjini. Ukifika stendi ya Msamvu panda magari yanayo kwenda Gairo Dodoma, shuka Njiapanda ya Berega (Kiegea) kutoka Kiegea hadi shuleni kuna umbali wa km 5 nauli ya pikipiki ni tsh 3000/=.

Ukitoka Kilosa Mjini panda magari ya kwenda Dodoma shuka Njiapanda ya Berega (Kiegea). kwa mabasi yanayotoka Kilosa mjini kwenda Morogoro kupitia Dumila, shuka Dumila panda magari ya kwenda Gairo kisha shuka njiapanda ya Berega (Kiegea) nauli hadi shuleni Tsh 3000/= kwa pikipiki. Kwa wazazi wanaotoka, Mikoa ya kanda ya ziwa, magharibi na kati, kupitia Dodoma kuelekea Morogoro, shuka njiapanda ya berega (Kiegea). Kwa wazazi wanaotoka Lindi, Mtwara, Dar es salaam,Arusha, Kilimanjaro,Tanga na Pwani panda mabasi yanayokwenda Dodoma shuka njia panda ya Berega(Kiegea).

**Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 13/1/2026 na mwisho wa kuripoti shuleni tarehe…………………**

Aidha Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **Elimu Na 25** ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 1.SARE YA SHULE.

i. Shati nyeupe mbili mikono mifupi na Tsh.2,000/= kwa ajili ya gharama ya kuweka nembo ya shule;
ii. Tai rangi ya damu ya mzee yenye mistari myeupe (zitapatikana maeneo ya karibu na shule kwa TSH.5000/= kwa atakayehitaji);
iii. Vest mbili nyeupe au nyeusi zisizo na mapambo za kuvalia ndani ya shati;
iv. kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu (albinism) waje na mashati ya mikono mirefu.
v. Sketi 2 rangi ya damu ya mzee (**redish brown)** Kitambaa daraja la 1 mshono linda box sketi ziwe ndefu zifike kwenye vifundo vya mguu
vi. Kwa wanafunzi wa kiislamu sketi iwe ndefu inayofika kwenye kifundo cha mguu na nusu kanzu nyeupe mikono mirefu (zisibane) na hijab zisizo na mapambo nyeupe zisipungue 2 na
vii. wanafunzi wa scout aje na sare za scout;
viii. Sweta rangi ya damu ya mzee lenye shingo ya **V**. inayofanana na sketi ya darasani unaweza kuja nayo au inapatikana maeneo karibu na shule;
ix. kwa wenye shida ya kifua waje na sweta ndefu( pull neck) inayofanana na sweta la shule/sketi ya darasani ambayo inavaliwa ndani ya sweta.

***ANGALIZO: ISIWE KINYUME NA RANGI TAJWA HAPO JUU***.

### 3. SARE YA KUSHINDIA KWA WANAFUNZI WOTE.

i. Tshirt 2 za rangi ya kijivu yenye kola (inajulikana kama form six);

ii. Skirt 2 rangi ya dark bluu mshono rinda box (zifike kwenye kifundo cha mguu na zisiburuze chini) kwa atakayehitaji zinapatikana karibu na shule;
iii. Hijab/mtandio mweupe usiokuwa na mapambo/urembo kwa wanafunzi wa kiislamu.

***N.B: HAIRUHUSIWI KABISA KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI NA SIKU YA KURIPOTI VAA SARE YA SHULE.***

4.**VIFAA VINGINE**

i. Godoro futi 2.5
ii. Shuka za sare 2 rangi ya bluu bahari na pink.(TETRON)
iii. Blanket;
iv. chandarua cha pembe nne cheupe;
v. Taulo,kitenge 1, .
vi. Tracksuit nyeusi ya michezo isiyobana (yenye mistari myeupe pembeni);
vii. Raba za michezo rangi yeyote.
viii. Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa na kamba matundu yasipungue manne;
ix. soksi nyeusi jozi mbili
x. Ndoo moja
xi. Galooni la lita 5 la kuhifadhia maji ya kunywa
xii. vifaa vya chakula (sahani, kijiko,kikombe na chupa ya mkononi ya maji ya kunywa darasani )
xiii. Madaftari makubwa counter book 12 kuanzia quire 3;
xiv. Madaftari madogo aina ya msomi 12;
xv. Rimu ya karatasi moja kila muhula isiyo na mistari kwa ajili ya photocopy aina ya **AONE,**
xvi. Kikokotozi (Calculator), mkebe wa hesabu,rula,ufutio,kalamu za wino za kutosha , graph paper;
xvii. kamusi ya kingereza;
*xviii.* Taa ya sola au tochi ni ***MUHIMU SANA UMEME UNAPOKATIKA KWA AJILI YA KUJISOMEA.***
*xix.* Nguo za ndani dazani moja( chupi na tights);

xx. Taulo za kike za kutosha;

xxi. Mafuta ya kupaka yasio na harufu kali (asije na vipodozi na vitu vingine vinavyochubua ngozi);

xxii. sabuni ya unga pkt 3 na ya mche miwili,

xxiii. toilet paper 3,

xxiv. Dawa ya mbu aina ya HT;

xxv. Kamba za kuanikia nguo pamoja na vibanio.

xxvi. Kwa wenye uhitaji maalumu (Albinism) mafuta na kofia vinapatikana shuleni kwa msaada wa serikali na wadau mbalimbali.

xxvii. Sanduku la bati imara na lenye kufuli mbili.

xxviii. Mwanafunzi mwenye ***BIMA YA AFYA YA NHIF*** aje nayo kwa ambao hawana aje na fedha kiasi cha **Tshs 50,400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima ya **afya ya NHIF** kupitia shuleni.

***NB - NI MUHIMU SANA KWANI TUPO KARIBU NA HOSPITAL YA BINAFSI INAYOPOKEA BIMA YA AFYA.***

5. **Vifaa vya usafi**

xxix. Fagio la chelewa 1 kwa ajili ya kufagilia eneo lake;

xxx. Sabuni ya chooni lita 1 ya kiwandani;

xxxi. Sqeezer 1 ya kukaushia maji au brush ya lungu ya kusugulia sink la choo1;

xxxii. Soft broom 1 ya kufagillia sakafu

.

**6. PAMOJA NA MAELEKEZO HAYO NAAMBATANISHA .**

1. Sheria, kanuni na taratibu za shule.
2. Fomu ya uthibitisho wa afya; medical certificate form.
3. Fomu ya kujiunga na shule na uthibitisho wa kukubali sheria.

**NB**; Muda wa kuripoti shule mwisho saa 11:30 jioni, kwa wanaotoka mbali tafadhali fika kwenye mji au mahali salama ulale kisha siku ya pili fika shuleni.

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MGUGU**

## 7.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

**S**hule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

## 7.1 KANUNI ZA LAZIMA KUFUATWA NA WANAFUNZI WOTE SHULENI

a) Kula chakula cha shule ni lazima kulingana na ratiba iliyopo labda kama kuna ushauri wa kitaalamu unaoshauri vinginevyo, ingawa shule haina special diet/ chakula maalumu kwa wagonjwa na shule ina balance diet.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule. Ikiwa na pamoja na; I. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation). II.Kuwahi katika kila shughuli za shule.

c) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya mazingira ya ndani ya shule

d) Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na Mazingira ya shule. Kuoga na kufua nguo ni lazima.

e) Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shule na wakati wa kusafiri kutoka na kurudi shuleni.

f) Kutunza Mali za Umma kwa uaminifu na kwa Uzalendo .

g) Heshima kwa viongozi ,Wazazi ,Wafanyakazi wote ,Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

**h)** Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na vitu vya thamani kubwa bwenini , ikiwa ni pamoja na kuwa na pesa nyingi bwenini au darasani ili kudhibiti wizi/**UNAWEZA**

**KUMFUNGULIA AKAUNTI YA NMB - WAKALA WA KUTOA PESA ANAPATIKANA MAENEO YA SHULE.**

i) Kufanya biashara ya aina yoyote kwa wanafunzi au mtu yoyote ndani ya eneo la shule,kukopesha pesa kwa wanafunzi au mtu yoyote kwa riba au bila riba ndani ya eneo la shule.

j) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni na Mwanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele na asinyoe upara/kiduku wala kuweka dawa yeyote kichwani.

k) Hakuna siku maalum ya kutembelea mwanafunzi, iwapo mzazi/ mlezi amepata nafasi ya kumtembelea mwanafunzi anaruhusiwa kuja siku ya Jumamosi kuanzia saa 7 mchana baada ya usafi na masomo binafsi na siku ya Jumapili baada ya ibada-wakati wa vipindi hairuhusiwi kumwona mwanafunzi, na mgeni ambaye hakuandikwa katika taarifa binafsi za mwanafunzi haruhusiwi.

l) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shuleni au kuletewa vyakula kutoka nyumbani.

m) Mwanafunzi asije na simu ya mkononi na viambata vyake,kuhifadhi simu kwa mwalimu na kutumia simu ya mwalimu kwa mawasliano. Mawasilianao muhimu yatafanywa na ofisi/kama atahitaji mawasiliano simu ya shule itatumika.

n) Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kujipamba kwa kitu chochote cha kuvaa au kujipaka, pia asifuge kucha

o) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha mbaya na ya matusi kwa wenzake na kwa mwanajumuiya yeyote

p) Ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele wakati wowote darasani / bwenini au kuondoka darasani bila ruhusa.

q) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuigia na majibu, maandishi katika mtihani na kuonesha majibu ya mtihani kwa mwanafunzi mwingine.

r) Si ruhusa kwa mwanafunzi kutembelea maeneo yafuatayo bila kibali: ofisi ya walimu(staff room), ofisi za shule, jikoni, chumba cha kompyuta, maabara na nyumba za watumishi.

s) Si ruhusa kwa mwanafunzi kununua vitu bwenini na hairuhusiwi kula vyakula bwenini

t) Si ruhusa kujichora TATUU mwilini
u) Kutoa taarifa ya ugonjwa kwa mzazi bila ruhusa ya mwalimu mlezi.
v) Kukaa na dawa bwenini bila kibali maalumu kutoka kwa mwalimu mlezi.
w) Si ruhusa kuwa na vitu hatarishi bwenini kama vile kisu.

**7.2) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

a) Wizi
b) Kumiliki simu au kutumia simu isiyo ya shule, kumiliki laini ya simu au chaji ya simu na viambatanisho vyote vinavyohusiana na simu
c) Utoro ikiwa ni pamoja na kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule au Kukosa kuhudhuria vipindi darasani au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi au kutohudhuria masomo kwa siku 90 bila taarifa au kwenda nje ya shule bila kibali.
d) Uasherati,Usagaji, kuoa au kuolewa na mahusiano ya jinsia moja
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanfunzi , Kumpiga mwalimu na mtumishi yoyote.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kugoma,kuchochea na kuhamasisha, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa Shule au Watu.
i) Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na Mwalimu.
j) Kufanya Jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua au kunywa sumu, kuua na yafananayo.
k) Kushiriki matendo ya kiharifu, siasa na matendo yoyote yanayo pelekea kuvunja sheria za nchi.
l) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako , walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
m) Kubadili dhehebu bila kibali cha mzazi/mlezi kwa maandishi.
n) Makosa yote ya jinai.
o) Kuvuka mto Mgugu/Berega unaozunguka eneo la bweni-mto huu ni hatari sana.

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI WAKATI WA KURIPOTI.**

Kila mwanafunzi ahakikishe anajaza kwa umakini fomu zifuatazo kabla ya kuja shuleni aidha mzazi unatakiwa kuipakua fomu hii, ya mwaka 2024 na kuinakilisha(print) kwa ajili kuisoma kwa makini na kukubaliana na taratibu na kujaza sehemu zote zinazopaswa kujazwa.

**KAMA KUNA SEHEMU HAIJAELEWEKA WASILIANA NA MKUU WA SHULE AU MAKAMU KUPITIA NAMBA ZILIZOPO UKURASA WA KWANZA JUU KULIA.**

***Aidha fomu zifuatazo ni lazima ziletwe shuleni zikiwa zimejazwa kwa ukamilifu wake.***

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

## 8.0 HITIMISHO

Hakikisha mzazi au mlezi umesoma kwa umakini fomu hii na kujadiliana na mwananao juu ya utayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii.

…………………………

BANDU KIPENZI

MKUU WA SHULE

# SHULE YA SEKONDARI YA MGUGU

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

1. **TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI ( picha 2 za mwanafunzi na picha za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni)**

A. Jina kamili la mwanafunzi

i. JINA LA KWANZA……………………………………

ii. JINA LA BABA……………………………………….

iii. JINA LA UKOO……………………………………..

B. Tarehe ya kuzaliwa………Mwezi………………Mwaka……………

**(Ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)**

C. Mahali alipozaliwa;

Kijiji/Mtaa…………………………..Kata …………………

Wilaya……………………………………..

Mkoa………………………….

D. Mwanafunzi huyu ni YATIMA au SIYO YATIMA. ( kama ni yatima eleza uyatima wake ni mzazi mmoja au wazazi wote)

………………………………………………………………………………………

E.Taarifa za shule ya msingi uliyosoma, ambazo zinzpatikana shule ya msingi uliyosoma.

i.Jina la shule………………………………….

ii.Namba ya mtihani ya darasa la saba…………………………….

iii.Prem namba ya mwanafunzi…………………………………

E. Mawasiliano ya mwanafunzi.

i. Namba ya simu 1……………………………………BABA/MLEZI
ii. Namba ya simu 2……………………………………MAMA/MLEZI
iii. Namba ya simu 3……………………………………Jirani
iv. Namba ya simu 4……………………………………Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa, UNAOISHI MZAZI/MLEZI-
Jina lake……………………Saini…………………….

muhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa…………………………...

**2. TAARIFA YA WAZAZI/ WALEZI**

a) Jina la Baba/mlezi…………………………………………………………………
b) Kazi ya baba/mlezi………………………………………………………………..
c) Namba ya Kitambulisho cha Taifa/NIDA ………………………………………………
d) Anwani ya Mzazi/mlezi
S.L.P………………………..ENEO…………………..
e) Jina la mama/ mlezi…………………………………..
f) Kazi ya mama/mlezi…………………………………..
g) Namba ya kitambulisho cha Taifa/Nida……………….
h) Anwani yake………………………………………
i) Ndugu wa karibu wanaoweza kuchukua jukumu badala WAZAZI/ ninao waruhusu kumtembelea/ kumsaidia mtoto wangu akiwa hapo shuleni ni (ANDIKA JINA, MAWASILIANO UHUSIANO WAKE NA PICHA YAKE)

i. JINA ………………………………uhusiano…………………..simu …………..
ii. JINA ………………………………uhusiano…………………..simu …………..
iii. JINA ………………………………uhusiano…………………..simu …………..
iv. JINA ………………………………uhusiano…………………..simu …………..
v. JINA …… ………………………uhusiano…………………..simu …………..

**BANDIKA PICHA ZAO HAPA CHINI KWA KUANDIKA KIWAKILISHI CHA NAMBA ZA HAPO JUU.**

**AHADI NA KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI YA MGUGU KIDATO CHA I** mwaka **2026** ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Mgugu.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumuita mzazi/ mlezi wangu.
v. Nadhibitisha kwamba nimepokea maagizo, na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia. …………………………………………… (Jina la mwanafunzi)

Saini ya mwanafunzi ………………….. Tarehe……………….

---

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi …………………………………………………………………………… ninakubali mtoto wangu Kupata na kupokea nafasi katika shule ya Sekondari Mgugu mwaka **2026**. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. **Na ninaahidi kufuatilia maendeleo yake ya kitaaluma na tabia kila muhula bila kukosa. Napenda ifahamike kuwa dini ya mwanafunzi ni……………………………........... Dhehebu lake………………………............**

**Anuani yangu ya kudumu…………….............**

Saini ya Mazazi/Mlezi………………… Tarehe…………… No ya simu……………

**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a Medical Officer of government hospital

1. Students' name…………………………………………………………...
2. Age years…………………………………………………………………...
3. Blood agunt (Red and white) ………………………………………………….
4. Stool Examination………………………………………………………..
5. Unarisis……………………………………………………………………….
6. Syphilis test……………………………………………………………...
7. T.B Test………………………………………………………………………
8. Filariasis……………………………………………………………………..
9. Chest:………………………………………………………………………….
10. Spleen…………………………………………………………………..
11. Abdomen…………………………………………………………………....
12. Sickle cell…………………………………………………………………..
13. Asthma……………………………………………………………………..
14. Blood group………………………………………………………………….

16.Eyes……………………………………………………………………..

17.Ears…………………………………………………………

**ADDITIONAL INFROMATION:** Eg Physical defector impairment infections, chronic or Familydiseases………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I certify that the above student is fit/ unfit for admission into a boarding/ day Secondary School

SIGNATURE……………………………………DESIGNATION………………………………
STATION…………………………………… DATE………………………… ….

MFANO WA MUUNDO WA SARE ZA SHULE





**Sare ya darasani**



**Sare ya kushindia**



**Sare ya kushindia**



**Sare ya michezo**